**Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – "Palipo na wazee"**
**"Mizozo na utatuzi-palipo na wazee"**
Kipindi cha 5: "Chimbuko la mkinzano"
AUTHOR: Chrispin Mwakideu
EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

## List of characters by scenes:

### SCENE ONE : RECONCILIATION AT THE RIVER BANK

- **Mitumba (m, 50)**
- **Lela (f, 20)**
- **Shani (f,17)**
- **Waliani (m, 75)**
- **Mixed group (at least 4 ppl)**

### SCENE TWO : SOMBA AND KERO MEET AT MILITARY HEADQUARTER

- **Somba (m, 55)**
- **Kero (f, 55)**

### SCENE THREE: SHANI, LELA AND GULU AT THE FARM IN KIJANI

- **Lela (f, 20)**
- **Shani (f,17)**
- **Gulu (m, 17)**
-

### SCENE FOUR: KERO AT PRESIDENT MATONGE 'S OFFICE

- **Kero (f, 55)**
- **Matonge (m, 65)**

**Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – "Palipo na wazee"**
**"Mizozo na utatuzi-palipo na wazee"**
Kipindi cha 5: "Chimbuko la mkinzano"
AUTHOR: Chrispin Mwakideu
EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

**MSIMULIZI**

**INTRO:**

Nawasalimu na karibuni katika kipindi cha Noa bongo! Jenga maisha yako. Hiki ni kipindi cha sita katika hadithi ya mizozano na jinsi ya kuitatua kwa njia za kitamaduni, iitwayo, **"Palipo na wazee".** Kipindi kilichopita, waTorube na wa Koroma wanaoishi bonde la Kijani walipatanishwa baada ya mkongwe Waliani kuwaongoza katika mapatano kimila. Wakati wuwo huwo, Somba, mkuu wa majeshi, na Kero, mkuu wa upelelezi, wanapanga kudhoofisha amani ya nchi yao kabla ya uchaguzi unaokaribia kwa kuwapatia silaha watu waTorube. Je mipango yao hiyo itafanikiwa ? Wacha tuone katika kipindi cha leo, " **Chimbuko la mkinzano".** Tunaanzia moja kwa moja katika kingo za mto wakati kila mtu anasubiri jawabu la Mitumba baada ya Masambo kumuomba awakubalie watoto wao kuoana kama ishara ya kuziunganisha jamii hizi kupitia ndoa.

**SCENE ONE: RECONCILIATION AT THE RIVER BANK**

| |
|---|
| **1. SFX: RIVER FLOWING SMOOTHLY DOWNSTREAM** |

| | |
|---|---|
| **2. MITUMBA:** | **(Loss for words)** Ah..ah..Sijui niseme nini. |
| **3. WALIANI:** | Siku za kale, makabila yalipokuwa yanapigana vita kila wakati, ndoa za mchanganyiko zilitumiwa kuleta maelewano. Lakini sasa mambo yamegeuka wazazi hawawachagulii tena wasichana wao wachumba. Hata hivyo muda umwekwenda. Watu wangerudi majumbani mwao. |

**4. SFX: MURMURS AND RANDOM TALK FROM CROWD (studio)**

| | |
|---|---|
| **5. SHANI:** | **(excited)** Sawa. |
| **6. LELA:** | Sawa nini? Hmm Shani? Kama unataka kuolewa na Gulu, olewa. Usinizungumzie mambo hayo tafadhali. |
| **7. SHANI:** | Sikuwa nataka kukuzungumzia. Lakini maadamu umeyaanza mwenyewe, wacha nichukuwe fursa hii. Umemsikia mzee Waliani, ni njia moja ya kuleta amani. |
| **8. LELA:** | Amani imeshapatikana, au ulikuwa umelala kwenye sherehe? |
| **9. SHANI:** | Unahitaji kuolewa Lela. La sivyo, mimi sitaweza. |
| **10. LELA:** | Aha, kwa hivyo ulikuwa una lengo lako. Unataka kuolewa! |
| **11. SHANI:** | La, ni sharti uolewe wewe kwanza, kisha mimi. Hivyo ndiyo mila inataka. |
| **12. LELA:** | Shani, baada ya mama kuchukuliwa, niliachiwa jukumu la kukulea. Nimejinyima mengi kuhakikisha kuwa wewe.. |
| **13. SHANI:** | **(Not amused)** Usinilaumu kwa ajili ya maisha yako Lela! |
| **14. MITUMBA:** | Eh eh eh! Ni lini nyinyi mutajuwa kuwa ni madada muliotoka tumbo moja? Tumetoka kupatana na waTorube, sasa kuzozana huku ni kwa nini? |
| **15. LELA:** | Pole baba. |

**16. MITUMBA:** Sawa. Lakini staki tena magombano.**(calmer)** Niambieni binti zangu, kuna mmoja wenu anataka kuolewa na wavulana wa Masambo?

**17. SHANI:** **(sarcastic)** Muulize Lela, yeye ndiye mkubwa.

**18. LELA:** Mkubwa? Mbona usijibu? Wewe ndiye umechachawa na kuolewa!

**19. MITUMBA:** Sawa. Hilo kwangu ni jawabu la Hapana. Sasa tunyamazeni na tudumishe amani kama alivyosema Waliani.

**20. MSIMULIZI:** Baada ya umati kuondoka mtoni, hewa ya amani, utulivu na maridhiano ilitanda katika bonde la kijani. Lakini baada ya siku chache, kule jijini, mikutano na kampeni za kisiasa zimeanza na kura za maoni zikionesha Rais anayetawala bwana Matonge hafanyi vizuri. Ilionekana alikuwa na kura asilimia 30 dhidi ya asilimia 70 za Roselyn . Kero, ambaye ndiye aliyekuwa wa kwanza kupata habari hizi,, alijua kuwa alitakiwa kuchukua hatua haraka, na alikuwa katika gari lake kwenye lango la makao makuu ya jeshi.

**SCENE TWO: SOMBA AND KERO MEET AT MILITARY HEADQUARTER**

| **21. SFX: CAR HOOTING..** |
|---|

**22. KERO:** **(Annoyed)** Ana shida gani huyu, mwanajeshi kiziwi nini? Haoni kwamba hii ni gari ya serikali na afungue lango haraka? Piga tena honi dereva! Piga honi kwa nguvu!

**23. SFX: HOOTING SEVERAL TIMES**

**24. KERO:** **(Very angry)** Sasa ndio anakuja kuchunguza kama tuko na mabomu? Somba anatoa wapi hawa wanajeshi? Ah, sitapoteza muda zaidi hapa.

**25. SFX: AUTOMATIC CAR WINDOW WINDS DOWN**

**26. KERO:** **(Command)** Wewe! Mlinzi mwanajeshi, fungua lango! Hujui mimi ni nani? Mimi ni Kero, mkuu wa upelelezi nchini na sio gaidi! Mimi ndiye huhakikisha magaidi hawaingii nchini!

**27. SFX: WIDE GATE OPENED**

**28. KERO:** Twende dereva ! Ondoa gari! Unasubiri nini?

**29. SFX: CAR DRIVES OFF SPEEDILY (inside)**

**30. KERO:** Simama! Mkuu wa majeshi Somba tayari ananisubiri!

**31. SFX: CAR SUDDENLY BRAKES TO A HALT (inside)**

**32. SOMBA:** Ala, Kero kuna dharura gani?

| **33. SFX: CAR DOOR OPENED AND SHUT QUICKLY (inside)** |
|---|

**34. KERO:** **(urgency)** Jenerali Somba, nimepata fununu fulani. Ni lazima tuendelee na mpango haraka!

**35. SOMBA:** **(Inviting)** Karibu afisini, tunaweza kuongea huku tukiburudika na kinywaji.

**36. KERO:** **(serious tone)** Sikujakuketi na kunywa kahawa Somba. Hali kwa hivi sasa imegeuka. Umenisikia nimesema nini?

**37. SOMBA:** **(hitting back)** Kero! Hii ni kambi yangu. Hapa kila mtu ananipa heshima! Itakulazimu utulie na useme na mimi kwa upole, au rudi garini kwako na urudi ulikotoka!

**38. KERO:** **(takes a deep breath)** Niwie radhi, mambo bwana. Matonge atapoteza kiti kama hatutafanya lakufanya. Umeziona kura za maoni kwa sasa?

**39. SOMBA:** **(calmly)** Kero, Matonge hatapoteza. Hawezi! Sisi ndiyo tunaamuwa ni nani anashinda, au anapoteza. Sio kura za maoni, sio wananchi, na hata siye rais mwenyewe. Tutembee..na unieleze ni nani anayekukoroga akili.

**40. MSIMULIZI:** Wakati marafiki hao wawili wakitembea na kuongea, katika bonde la Kijani, Maisha yalikuwa ya amani, na umakinifu. Kila mmoja alijuwa thamani ya maisha. Masambo keshamlipa Mitumba vichwa kadha vya ng’ombe kama fidia ya kosa lake, na Mitumba pia kesha mpa fidia

yake Masambo baadhi ya mazao yake na kuiondolea mbali milingoti aliyoikita awali. Sasa tuelekee shambani, waliko Shani na Lela ambao wako makini wakifanya kazi yao, pamoja na Gulu, aliyetumwa na baba yao Masambo awasaidie.

**SCENE THREE: SHANI, LELA AND GULU AT THE FARM IN KIJANI**

| 41. **SFX: PLANTING SEEDS IN THE GROUND/ Sound of harrow + hoe/farm sounds (birds, animals..)** |
|---|

**(Laughter from Shani and Lela)**

| | |
|---|---|
| **42. SHANI:** | Gulu..Umewahi kupanda mbegu hapo awali? Umezitupa nyingi nje ya mashimo.**(more laughter)** |
| **43. LELA:** | Shani usimcheke. Nina hakika anatia juhudi kujifunza. |
| **44. GULU:** | Asante. Kesho nitakualika kwetu uje ukamue ng’ombe maziwa ili na mimi nikucheke. |
| **45. SHANI:** | Ati!? Hapana ..siwezi kukakua ng’ombe. Nitapigwa teke. |
| **46. LELA:** | Si ni vizuri kuwa tunafanya kazi pamoja? WaTorube na waKoroma? Singesadiki siku hii ingelifika. |
| **47. SHANI:** | Hata mimi. Labda sasa pia tungekula suluhu na waasi wa Kimbebe ambao wamekuwa wakiiba ng’ombe za watu wenu Gulu. |
| **48. GULU:** | Sidhani. |
| **49. LELA:** | Mbona umesema hivyo Gulu? Baada ya watu wangu |

kupatana na watu wako. Naamini taifa zima linaweza kupatanishwa. Tunayehitaji ni mtu kama Waliani.

**50. GULU:** Hakuna suluhu na watu wa Kimbebe. Nilielezwa hivyo. Wametupa misiba na masika mingi . Tena isitoshe dini yao ni tofauti.

**51. SHANI:** Kwa hivyo dini ndio kizingiti cha kuleta amani? Nilifikiri dini zote zililetwa kwa ajili ya kuhubiri amani.

**52. GULU:** Kweli, ni sadiki. Lakini, moja ya sababu yao ya kupinga serikali ni kwa sababu ya dini..

**53. SHANI:** Nafikiri Waliani angelitumiwa kuleta uwiano kati ya waasi wa Kimbebe na serikali.

**54. GULU:** **(Adamant)** Huelewi Shani! Hilo si jambo dogo. Hawa wana silaha zinzotumiwa na wanajeshi. Nilikuwepo walipoiba ng'ombe zetu. Lakini tuna imani tutaziregesha!

**55. SHANI:** Kivipi? Umesema wana silaha kama za wanajeshi?

**56. MSIMULIZI:** Naam, mpenzi msikilizaji. Utapiganaje na adui hatari kama huyo? Lakini jibu liko njiani laja. Kule kando kabisa jijini, Rais alikua na wakati mgumu kumuelewa mkuu wa upelelezi, Kero, aliyekuwa akimueleza. Hebu tujiunge nao katika afisi ya Rais..

**<u>SCENE FOUR: KERO AT PRESIDENT MATONGE 'S OFFICE</u>**

**57. SFX: PEN HITTING ON TABLE WHEN SOMEONE IS NERVOUS (studio)**

**58. MATONGE:** Kero, Wacha kudona dona meza yangu kwa kalamu.

Unanikera!

**59. KERO:** Samahani. Mheshimiwa rais, ni vile nina hofu kwa yale yanayotokea.

**60. MATONGE:** **(Disbelief)** WaTorube na waKoroma wamepatana? Kero una hakika?

**61. KERO:** Kabisa. Mzee mmoja anaitwa Waliani amewapatanisha kimila. Yaaminika, wanaume wote wa kabila hizo mbili waliokuwa wamekwenda vitani hapo bondeni, walirudi nyumbani wakiwa na amani. Wanaimba kwa furaha na hata silaha zao wakazitia moto.

**62. MATONGE:** **(marveling)** Inashangaza! Kama ndoto. Kwanini watu kama hao wasitumiwe katika bara letu kutumia vipawa vyao ili kuleta amani katika bara letu.

**63. KERO:** Mheshimiwa, huu sio wakati wa amani. Uko kwenye vita! Tuna kazi ngumu mbele yetu kuhakikisha umebaki madarakani.

**64. MATONGE:** **(Hesitant)** Lakini Kero, ombi lako la kutaka kuwapa silaha waTorube halina tena uzito kwa sasa. Wana amani. Wanataka amani.

**65. KERO:** Wamepatanishwa na wa Koroma. Na sio na waasi wa Kimbebe. Kama tutaanza kugawanya bunduki leo basi hujui kesho kutaamka vipi? Tusipochangamka, labda hata wanaweza kula suluhu na waKimbebe na kuipenduwa serikali yako.

**66. MATONGE:** **(Given in)** Sawa! Haya! Endelea,kamwambie Somba

awape silaha waTorube. Kuweni makini.

**67. KERO:** **(grateful)** Usiwe na shaka, muheshimiwa. Nitatoa taarifa kwa umma kwamba tunafanya hivi kuwalinda wananchi wetu kutokana na waasi na wezi walioingia nchini kimakosa. Hakuna atakayejuwa.

**68. MATONGE:** Na huyu mzee Waliani? Unafikiri anaweza kuwasihi waasi wa Kimbebe nao walete maridhiano?

**69. KERO:** Niachie mimi. Usihofu. Vile umeniamuru, tutatekeleza. Siku njema.

**70. SFX: DOOR CLOSED BEHIND**

**<u>OUTRO:</u>**

Huku mlango wa Rais ukifungwa, nasi tunafikia mwisho wa kipindi hiki cha sita cha mizozo na utatuzi. Kutatokea nini tena? Ambapo sasa Rais Matonge ameruhusu waasi waTorube wapewe silaha? Kero naye anapanga kumfanyia nini mpatanishi wa amani mzee Waliani? Kwa haya na zaidi, usikose kusikiliza kipindi kifuatacho. Kama unataka kusikiliza tena kipindi hiki, au kingine kilicholetwa na Noa bongo! Jenga maisha yako, tembelea tovuti yetu www.dw.de/kiswahili

Kwaheri kwa sasa.